

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA NISHATI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



**KUMB: PPR/2024 - 08/01**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA  
PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 7 AGOSTI 2024**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini zitakazotumika kuanzia **Jumatano ya tarehe 7 Agost 2024 saa 6:01 usiku**. Kwa mwezi Agost 2024, bei za rejareja na za jumla katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na. 1 na 2**, mtawalia.

**Jedwali 1:** Bei Kikomo za Rejareja (Shilingi/Lita)

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	3,231	3,131	3,257
Tanga	3,229	3,138	3,303
Mtwara	3,304	3,140	3,329

**Jedwali 2:** Bei Kikomo za Jumla (Shilingi/Lita)

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	3,099.16	2,998.89	3,124.84
Tanga	3,097.40	3,005.64	-
Mtwara	3,101.82	3,007.77	-

Bei za mafuta za rejareja kwa maeneo mbalimbali ya miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4**.

**MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA YALIYOSAFISHWA KATIKA SOKO LA DUNIA**

Bidhaa za mafuta zinazoagizwa na kupokelewa hapa nchini zinazingatia bei za mafuta katika soko la Uarabuni kwa bidhaa zenye viwango vya ubora vinavyokubalika nchini. Mwezi Agosti 2024, bei kikomo za mafuta zimekokotolewa kwa kuzingatia bei za soko la Uarabuni za mwezi Julai 2024. Kwa kulinganisha na bei za Juni 2024, bei za petroli zimeongezeka kwa 6.3% na bei za dizeli zimeongezeka kwa 2.2%.

## MWENENDO WA GHARAMA ZA UAGIZAJI

Gharama za uagizaji wa mafuta (*premiums*) zimeongezeka kwa wastani wa asilimia 3.58 kwa petroli na asilimia 4.35 kwa dizeli na kupungua kwa asilima 7.45 kwa mafuta ya taa katika Bandari ya Dar es Salaam; zimepungua kwa wastani wa asilimi 6.75 kwa petroli na dizeli katika Bandari ya Tanga; na pia zimepungua kwa wastani wa asilimia 7.54 kwa mafuta ya petroli na dizeli katika Bandari ya Mtwara.

## GHARAMA ZA BIDHAA ZA MAFUTA NCHINI

Gharama za bidhaa za mafuta zinajumuisha bei ya mafuta katika soko la dunia na gharama za uagizaji (*premiums*) ambazo ni gharama za usafirishaji, bima na gharama na faida za mleta mafuta kabla ya kodi, tozo na gharama nyingine za hapa nchini. Wastani wa gharama za bidhaa za mafuta yaliyofikishwa nchini zimeainishwa katika **Jedwali Na.3** baada ya kujumuisha gharama za mafuta katika maghala, yatakayopokelewa Agosti 2024 na uwianisho wa gharama za mafuta katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

**Jedwali Na. 3:** Wastani wa Gharama za Mafuta Yanapokelewa Bandarini (Shilingi/Lita)

Mwezi	Petroli	Dizeli	Mafuta Taa
Agosti 2024	1,873.23	1,901.31	2,046.71
Julai 2024	1,856.21	1,889.43	2,199.79
Tofauti	17.02	11.88	-153.08
Mabadiliko (%)	0.92%	0.63%	-6.96%

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

Gharama za mafuta yanayopokelewa (bei za mafuta katika soko la Uarabuni (FOB) na gharama za uagizaji (*premiums*) zinalipiwa kwa kutumia fedha za kigeni ikiwemo Dola ya Marekani na sarafu za nchi nyingine. Kwa bei za mwezi Agosti 2024, wastani wa gharama za kubadilisha fedha za kigeni (*Applicable Exchange Rate*) umepungua kwa asilimia **1.19** kutokana na *adjustment factor*

Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika **Jedwali Na. 4**. Aidha, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika **Jedwali Na. 2. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

EWURA inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kuzingatia yafuatayo: -

- bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupungua na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta.
- Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa **bei hizo zisizidi bei kikomo (*Price cap*) au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa (*Floor Price*)** kama zilivyokokotolewa kwa mujibu wa **Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa tarehe 28 Januari 2022 kupitia Gazeti la Serikali Na. 57 na marekebisho ya Kanuni tajwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 761A la tarehe**

**30 Oktoba 2023 na Mabadiliko ya Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja za Mwaka 2024.**

- d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana yakionesha bei za mafuta, punguzo, vivutio vya kibiashara vinavyotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- e) Wauzaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa stakabadhi za mauzo kutoka kwenye *Electronic Fiscal Pump Printers (EFPP)* na wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora unaotakiwa. Stakabadhi hizo pia zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya bidhaa za mafuta ya petroli.

**JEDWALI NA. 4: BEI KIKOMO ZA REJAREJA – SHILINGI/LITA**

<b>Na</b>	<b>Mji</b>	<b>Petroli</b>	<b>Dizeli</b>	<b>Mafuta Ya Taa</b>
1	<b>Dar es Salaam</b>	<b>3,231</b>	<b>3,131</b>	<b>3,257</b>
2	<b>Arusha</b>	<b>3,286</b>	<b>3,194</b>	<b>3,341</b>
3	Arumeru (Usa River)	3,286	3,194	3,341
4	Karatu	3,304	3,213	3,359
5	Longido	3,297	3,205	3,352
6	Monduli	3,291	3,200	3,346
7	Monduli-Makuyuni	3,296	3,204	3,351
8	Ngorongoro (Loliondo)	3,371	3,279	3,432
9	<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>3,236</b>	<b>3,136</b>	<b>3,261</b>
10	Bagamoyo	3,242	3,142	3,268
11	Bagamoyo (Miono)	3,273	3,173	3,298
12	Bagamoyo (Mbwewe)	3,254	3,154	3,279
13	Chalinze Junction	3,245	3,145	3,271
14	Chalinze Township (Msata)	3,250	3,149	3,275
15	Kibiti	3,252	3,151	3,277
16	Kisarawe	3,238	3,138	3,264
17	Mkuranga	3,241	3,141	3,266
18	Rufiji	3,259	3,159	3,284
19	<b>Dodoma</b>	<b>3,290</b>	<b>3,190</b>	<b>3,315</b>
20	Bahi	3,297	3,197	3,323
21	Chamwino	3,285	3,185	3,311
22	Chemba	3,316	3,216	3,342
23	Kondoa	3,323	3,223	3,348
24	Kongwa	3,287	3,187	3,313
25	Mpwapwa	3,291	3,191	3,317
26	Mpwapwa (Chipogoro)	3,303	3,203	3,329
27	Mtera (Makatopora)	3,309	3,209	3,334
28	Mvumi	3,296	3,196	3,322
29	<b>Geita</b>	<b>3,397</b>	<b>3,296</b>	<b>3,422</b>
30	Bukombe	3,386	3,285	3,411
31	Chato	3,418	3,318	3,443
32	Mbogwe	3,435	3,335	3,460
33	Nyang'hwale	3,412	3,311	3,437
34	<b>Iringa</b>	<b>3,295</b>	<b>3,195</b>	<b>3,321</b>
35	Ismani	3,301	3,200	3,326
36	Kilolo	3,300	3,200	3,325
37	Mufindi (Mafinga)	3,305	3,205	3,331
38	Mufindi (Igowole)	3,314	3,214	3,339
39	Mufindi (Mgololo)	3,317	3,217	3,343
40	<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>3,447</b>	<b>3,347</b>	<b>3,472</b>
41	Biharamulo	3,421	3,321	3,447
42	Karagwe (Kayanga)	3,463	3,363	3,489
43	Kyerwa (Ruberwa)	3,469	3,369	3,494
44	Muleba	3,447	3,347	3,472
45	Ngara	3,435	3,334	3,460
46	Misenyi	3,455	3,355	3,481
47	<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>3,389</b>	<b>3,289</b>	<b>3,414</b>
48	Mlele (Inyonga)	3,371	3,270	3,396
49	Mpimbwe (Majimoto)	3,408	3,308	3,434
50	Tanganyika (Ikola)	3,407	3,307	3,432
51	<b>Kigoma</b>	<b>3,394</b>	<b>3,293</b>	<b>3,419</b>
52	Uvinza (Lugufu)	3,384	3,284	3,409

53	Muyobozi Village (Uvinza)	3,396	3,295	3,421
54	Ilagala Village (Uvinza)	3,398	3,298	3,424
55	Buhigwe	3,392	3,292	3,418
56	Kakonko	3,394	3,294	3,420
57	Kasulu	3,403	3,303	3,428
58	Kibondo	3,400	3,300	3,426
59	<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>3,276</b>	<b>3,184</b>	<b>3,330</b>
60	Hai (Bomang'ombe)	3,279	3,187	3,334
61	Mwanga	3,269	3,177	3,324
62	Rombo (Mkuu)	3,292	3,201	3,351
63	Same	3,262	3,170	3,317
64	Siha (Sanya Juu)	3,282	3,191	3,337
65	<b>Lindi</b>	<b>3,290</b>	<b>3,153</b>	<b>3,316</b>
66	Lindi-Mtama	3,308	3,158	3,334
67	Kilwa Masoko	3,265	3,177	3,291
68	Liwale	3,311	3,189	3,337
69	Nachingwea	3,319	3,173	3,345
70	Ruangwa	3,321	3,180	3,346
71	<b>Manyara (Babati)</b>	<b>3,320</b>	<b>3,228</b>	<b>3,379</b>
72	Hanang (Katesh)	3,331	3,239	3,390
73	Kiteto (Kibaya)	3,335	3,244	3,390
74	Mbulu	3,333	3,241	3,392
75	Simanjiro (Orkasumet)	3,352	3,260	3,411
76	<b>Mara (Musoma)</b>	<b>3,397</b>	<b>3,297</b>	<b>3,422</b>
77	Musoma Vijijini (Busekela)	3,410	3,310	3,435
78	Rorya (Ingirijuu)	3,404	3,304	3,429
79	Rorya (Shirati)	3,412	3,312	3,437
80	Bunda	3,388	3,288	3,414
81	Bunda (Kisorya)	3,401	3,301	3,426
82	Butiama	3,394	3,294	3,420
83	Serengeti (Mugumu)	3,405	3,305	3,431
84	Tarime	3,406	3,305	3,431
85	Tarime (Kewanja/Nyamongo)	3,411	3,311	3,437
86	<b>Mbeya</b>	<b>3,338</b>	<b>3,238</b>	<b>3,364</b>
87	Chunya	3,348	3,248	3,373
88	Chunya (Makongolosi)	3,353	3,253	3,379
89	Chunya (Lupa Tingatinga)	3,355	3,255	3,381
90	Kyela	3,354	3,254	3,380
91	Mbarali (Rujewa)	3,322	3,222	3,348
92	Rujewa (Madibira)	3,336	3,236	3,361
93	Rujewa (Kapunga)	3,332	3,232	3,358
94	Rungwe (Tukuyu)	3,347	3,247	3,373
95	Busokelo (Iwangwa)	3,351	3,250	3,376
96	<b>Morogoro</b>	<b>3,256</b>	<b>3,156</b>	<b>3,282</b>
97	Mikumi	3,272	3,172	3,297
98	Kilombero (Ifakara)	3,294	3,194	3,320
99	Kilombero (Mlimba)	3,316	3,216	3,342
100	Kilombero (Mngeta)	3,306	3,205	3,331
101	Ulanga (Mahenge)	3,305	3,205	3,330
102	Malinyi	3,315	3,215	3,340
103	Kilosa	3,275	3,174	3,300
104	Gairo	3,275	3,174	3,300
105	Mvomero (Wami Sokoine)	3,267	3,166	3,292
106	Mvomero (Sanga Sanga)	3,256	3,156	3,282
107	Turian	3,281	3,181	3,307

108	<b>Mtwara</b>	<b>3,304</b>	<b>3,140</b>	<b>3,329</b>
109	Nanyumbu (Mangaka)	3,353	3,176	3,378
110	Masasi	3,329	3,156	3,355
111	Newala	3,336	3,161	3,361
112	Tandahimba	3,329	3,154	3,354
113	Nanyamba	3,329	3,154	3,354
114	<b>Mwanza</b>	<b>3,381</b>	<b>3,281</b>	<b>3,407</b>
115	Kwimba	3,399	3,299	3,425
116	Magu	3,389	3,289	3,415
117	Misungwi	3,376	3,276	3,401
118	Misungwi (Mbarika)	3,386	3,286	3,411
119	Sengerema	3,414	3,314	3,439
120	Ukerewe	3,441	3,341	3,466
121	<b>Njombe</b>	<b>3,324</b>	<b>3,224</b>	<b>3,349</b>
122	Luponde	3,330	3,230	3,355
123	Njombe (Kidegembye)	3,344	3,244	3,370
124	Ludewa	3,362	3,261	3,387
125	Makambako	3,316	3,216	3,341
126	Makete	3,355	3,254	3,380
127	Wanging'ombe (Igwachanya)	3,321	3,221	3,347
128	<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>3,404</b>	<b>3,304</b>	<b>3,430</b>
129	Sumbawanga Rural (Mtowisa)	3,404	3,304	3,430
130	Kalambo (Matai)	3,411	3,311	3,437
131	Nkasi (Namanyele)	3,418	3,318	3,443
132	Kabwe	3,432	3,332	3,458
133	Nkasi (Kirando)	3,427	3,327	3,453
134	<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>3,355</b>	<b>3,225</b>	<b>3,380</b>
135	Mbinga	3,367	3,238	3,393
136	Namtumbo	3,360	3,216	3,385
137	Nyasa (Mbamba Bay)	3,377	3,263	3,403
138	Tunduru	3,334	3,191	3,360
139	<b>Shinyanga</b>	<b>3,360</b>	<b>3,260</b>	<b>3,386</b>
140	Kahama	3,365	3,264	3,390
141	Kishapu	3,368	3,268	3,394
142	Ushetu (Nyamilangano)	3,376	3,276	3,402
143	Ushetu (Kangeme Village)	3,382	3,282	3,408
144	Salawe	3,374	3,274	3,399
145	<b>Simiyu (Bariadi)</b>	<b>3,378</b>	<b>3,278</b>	<b>3,404</b>
146	Busega (Nyashimo)	3,390	3,290	3,416
147	Itilima (Lagangabilili)	3,378	3,278	3,404
148	Maswa	3,372	3,272	3,397
149	Meatu (Mwanhuzi)	3,383	3,283	3,408
150	<b>Singida</b>	<b>3,322</b>	<b>3,222</b>	<b>3,347</b>
151	Iramba	3,334	3,234	3,360
152	Manyoni	3,307	3,206	3,332
153	Itigi (Mitundu)	3,322	3,222	3,348
154	Ikungi	3,317	3,217	3,343
155	Mkalama (Nduguti)	3,346	3,246	3,372
156	<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>3,348</b>	<b>3,247</b>	<b>3,373</b>
157	Songwe (Mkwajuni)	3,354	3,254	3,380
158	Ileje	3,351	3,251	3,377
159	Momba (Chitete)	3,357	3,257	3,382
160	Tunduma	3,352	3,252	3,377
161	<b>Tabora</b>	<b>3,339</b>	<b>3,239</b>	<b>3,365</b>
162	Igunga	3,339	3,239	3,365

163	Kaliua	3,352	3,252	3,378
164	Ulyankulu	3,350	3,250	3,375
165	Nzega	3,350	3,250	3,375
166	Sikonge	3,348	3,248	3,374
167	Urambo	3,349	3,249	3,375
168	Uyui	3,346	3,246	3,371
169	Mpyagula	3,371	3,271	3,397
170	<b>Tanga</b>	<b>3,229</b>	<b>3,138</b>	<b>3,303</b>
171	Handeni	3,250	3,158	3,282
172	Kilindi	3,265	3,173	3,317
173	Korogwe	3,242	3,150	3,296
174	Lushoto	3,251	3,160	3,306
175	Lukozi	3,257	3,165	3,311
176	Bumbuli	3,260	3,168	3,314
177	Mkinga (Maramba)	3,236	3,145	3,317
178	Muheza	3,234	3,143	3,303
179	Pangani	3,237	3,145	3,309

Dkt. James A. Mwainyekule  
**MKURUGENZI MKUU – EWURA**